

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/ AGOSTI 2013

MUDA: SAA 2½

**TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA LAIKIPIA  
(LENOCET) MWAKA WA 2013  
CHETI CHA KU HITIMU ELIMU YA SEKONDARI**

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2½

**MAAGIZO**

- (a) Jibu maswali manne pekee.
- (b) Swali la kwanza ni la lazima.
- (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Hadithi fupi.
- (d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- (e) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## SEHEMU YAA: FASIHI SIMULIZI

### Swali la lazima

1. a) (i) Maghani ni nini? (alama 2)  
(ii) Taja na ueleze vipera vinne vya maghani. (alama 8)
- b) Taja na ufafanue matumizi ya ngomezi nne za kisasa. (alama 4)
- c) (i) Eleza njia nne za ukusanyaji wa fasihi simulizi. (alama 4)  
(ii) Eleza udhifu katika uhifadhi wa kale wa fasihi simulizi. (alama 2)

## SEHEMU YAB: RIWAYA

### SAID A. MOHAMMED: *Utengano*

Jibu swali la 2 au la 3

2. “Mimi nilidhani tutagaiwa majumbo ..... nilifikiri tutakapopata uhuru wetu.....”
  - a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
  - b) Eleza jinsi ambavyo matarajio ya uhuru hayakutimia katika riwaya ya utengano. (alama 8)
  - c) Taja mhusika mmoja ambaye alinufaika zaidi na uhuru na ujadili sifa zake. (alama 8)
3. Fafanua chimbuko la utengano na athari za utengano huo kwa kurejelea riwaya ya utengano. (alama 20)

## SEHEMU YA C: TAMTHILIA

### TIMOTHY M. AREGE: *Mstahiki Meya*

Jibu swali la 4 au la 5

4. “Sina pingamizi maana hii ni “grand idea” lakini kwanza mniahidi hili mtakwenda nalo kaburini.”
  - a) Fafanua mukhtadha wa maneno haya. (alama 8)
  - b) Eleza mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
  - c) Taja na ufafanue maudhui mawili yanayotawala katika dondoo hili. (alama 6)
  - d) Taja sifa nne zinazohitishwa kuwa msemaji ni mhusika hasidi. (alama 4)
  - e) Ni jambo gani lililosababisha kuanza kwa mpango unaojadiliwa hapa. (alama 2)
5. Eleza matatizo ya wananchi wa mji wa Cheneo na athari zake. (alama 20)

## SEHEMU YAD: USHAIRI

Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali:-

### SHAIRI

1. Tunda la elimu, wasema wanazuoni,  
Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani,  
Ndipo hadhi apate, akumbukwe duniani.
2. Elimu bila ukweli, haizidi asilani,  
Giza na nuru muhali, katu havitengamani,  
Uwongo uje kwa ukweli, itue nuru moyoni.

3. Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani,  
Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni,  
Elimu njema miali, iangazayo gizani.
4. Mtu hachomwi na mwiba, na vifvu mguuni,  
Ulimwengu una miiba, tele tele majiani,  
Elimu jambo adhima, aso nayo maskini.
5. Wafu ni wasiosoma, watazika ardhini,  
Hai ndio waulama, wapaa maangani,  
Elimu jambo adhima, aso nayo maskini.
6. Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni,  
Pole uitafutapo, ujira usitamani,  
Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.
7. Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni,  
Wao wameongolewa, na ni taa duniani.  
Kweli wanapoiua watoe bila kuhini.
8. Elimu bila amani, mti usio majani,  
Haumtii kivuli, aukaliaye chini,  
Inakuwa mushkeli, wa kushuri insani.

### **SHAIRI B**

Inakera moyo  
Hii anga ambayo  
Huwasonya njiani  
Watokao mashambani  
Wa kusalimu kwa bashasha  
Wanaoshinda kivulini

Chini ya mwembe  
Wa umma.

Inakera moyo  
Hii sebule ambayo  
Huwahini mezani  
Wagotao nyundo kutwa  
Wa kukabili chakula  
Wanastarehe daima

Chini ya paa  
La umma.

**6. Maswali.**

- a) Pendekeza kichwa kifaacho kwa kila shairi la A or B. (alama 2)
- b) Haya mashairi ni ya aina gani? (alama 2)
- c) Taja sifa zozote tatu za kishairi katika shairi la B. (alama 3)
- d) Taja mbinu ya lugha ilivyotumiwa:-  
(i) Katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa sita katika shairi la A. (alama 1)  
(ii) Katika ubeti wa nne wa shairi la B. (alama 1)
- e) Fafanua kwa mukhtasari maudhui ya mashairi yote mawili. (alama 2)
- f) Andika ubeti wa mwisho wa shairi la A katika lugha nathari. (alama 3)
- g) Taja na uonyeshe jinsi idhini ya ushairi ilivyotumika katika shairi la A. (alama 4)
- h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika mashairi haya. (alama 2)  
(i) Waulama  
(ii) Wagotao

**SEHEMU YA E: HADITHI FUPI.**

**KEN WALIBORA NA SAID A. MOHAMED (*Wahariri*) - *Damu Nyeusi na hadithi nyingine.***

Jibu swali la 7 au 8

**7. *Ken walibora - Damu Nyeusi***

Fafanua jinsi ubaguzi wa rangi unavyodhihirika katika hadithi ya Damu Nyeusi. (alama 20)

**8. *Mohamed Said Abdala - Mke wangu***

Eleza mambo muhimu yanayochangia kuimarika kwa ndoa. (alama 20)